


Unapenda aina gani ya muziki?



✎ Espen Stranger-Johannessen
✉ Sara Rumen Krotev
📧 Jacob Haule
🗨️ 2
🗨️ Kiswahili! SW



LIDA Stories


lidastories.net

Unapenda aina gani ya muziki?

✎ Espen Stranger-Johannessen

✉ Sara Rumen Krotev

📧 Jacob Haule



This work is licensed under a Creative Commons


[Attribution 4.0 International License.](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0)

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>



Tulima anapenda muziki. Huwa
anasikiliza kila siku.


Rafiki zake, Carlos na Anita pia wanapenda muziki.






“Tulima, unapenda muziki wa aina gani?” Carlos anauliza.

“Ninapenda muziki wa
kimagharibi, lakini ninapenda
zaidi muziki wa nchi yangu,
Ethiopia.”




Wewe, unapenda muziki wa
aina gani?





“Ninatokea Kolombia.
Ninasikiliza salsa tu. Ni mzuri
kwa kucheza,” anasema Carlos.



Anita anasema, “Ninapenda
nyimbo za mapenzi na muziki
unaonifanya nifurahi.”